# HOTUBA YA DKT. ALLY POSSI – MWENYEKITI WA BARAZA KATIKA UFUNGUZI WA MKUTANO WA KWANZA WA BARAZA LA PILI LA WAFANYAKAZI WA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25 ILIYOTOLEWA TAREHE 10 OKTOBA, 2024 KATIKA UKUMBI WA TAKWIMU, MKOANI DODOMA

**Bi. Alice Mtulo, Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bi. Zuhura Kussaga, Katibu wa Baraza la Wafanyakazi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bw. Stanley Mahenge, Makamu Katibu wa Baraza la Wafanyakazi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bw. Mtani Songorwa, Mwenyekiti wa TUGHE Tawi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**
**Mwakilishi wa Vyama vya Wafanyakazi;**
**Mwakilishi wa TUGHE Ngazi ya Mkoa Dar es Salaam;**
**Viongozi wa TUGHE Tawi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**
**Wajumbe wote wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**
**Sekretariet ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**
**Waandishi wa Habari;**
**Mabibi na Mabwana**;

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania………***

**SOLIDARIIIITY …**

**MSHIKAMANOOO…**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutupa nguvu na afya ya kutuwezesha kukutana siku ya leo.

Ni furaha na heshima kubwa kwangu kusimama mbele yenu leo hii kama Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Hivyo, naomba kwa upekee kabisa kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kunipa wadhifa ya kuongoza Ofisi hii ya Wakili Mkuu wa Serikali kama Wakili Mkuu wa Serikali. Naahidi nitatekeleza majukumu yangu kwa weledi mkubwa.

Nashukuru kwa wafanyakazi wote kwa kunikaribisha katika Ofisi hii na ninaomba ushirikiano wenu kwenye kutekeleza majukumu yetu.

Nampongeza Dkt. Boniphace Luhende aliyekuwa Wakili Mkuu wa Serikali na Bi. Sarah Mwaipopo, aliyekuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri waliyofanya katika kipindi walichokuwepo katika Ofisi hii. Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza pia watumishi kwa kazi nzuri wanazoendelea kufanya.

## Ndugu wajumbe wa Baraza;

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa ikitekeleza majukumu yake ya kuratibu, kusimamia, na kuendesha mashauri yote ya Madai na Usuluhishi yanayofunguliwa dhidi au kwa niaba ya Serikali na Taasisi zake ndani na nje ya Nchi.

Katika kutekeleza majukumu hayo ofisi inazingatia Katiba, Sheria, Kanuni, Taratibu, na Miongozo mbalimbali inayosimamia shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ili kutimiza majukumu hayo nyeti ambayo Ofisi hii imekasimiwa, Baraza hili muhimu linajukumu la kipekee la kuendeleza mazingira ya kazi yenye tija, ushirikiano, na maendeleo ya wafanyakazi, ambao ndio uti wa mgongo wa mafanikio yetu. Tunapokutana hapa, ni fursa ya kipekee ya kutafakari mafanikio, kujadili changamoto, na kuweka mikakati ya pamoja kwa mustakabali wa Ofisi yetu.

## Ndugu wajumbe wa Baraza;

Nimeelezwa kuwa pamoja na masuala mengine kikao hiki cha Baraza la Wafanyakazi kina lengo la kufanya tathmini ya utendaji wa ofisi kwa mwaka uliopita kwa kuangalia malengo yaliyopangwa,

utekelezaji wa majukumu, changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji na Mikakati ya kukabiliana na changamoto husika. Hivyo, ni rai yangu kuwa sisi kama wawakilishi wa watumishi wenzetu tutakuwa mstari wa mbele kwenye kudadavua na kutoa mawazo chanya kwenye hoja mbalimbali zitakazojadiliwa leo hii. Tuwe huru kutoa hoja na sisi tutazipokea na kuzifanyia kazi

**Ndugu wajumbe wa Baraza;**

Kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/24, tumeshuhudia mafanikio mengi katika ofisi yetu. Mafanikio hayo ni-

i. Kuiwakilisha Serikali na Taasisi zake kwa ufanisi katika mashauri ya Madai na Usuluhishi ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hili, Ofisi imeweza kuokoa fedha mbalimbali ambazo Serikali ingetakiwa ilipe iwapo ingeshindwa mashauri hayo.

ii. Ofisi pia imengoza na kushiriki katika Timu za Serikali za Majadiliano (GNT) na kufanikisha kumaliza mashauri/migogoro nje ya Mahakama;

iii. Pamoja na kuhitimisha mashauri ya madai yasiyohusisha fedha yakiwemo mashauri ya katiba, haki za binadamu, uwekezaji na biashara yakiwemo:-

a. Shauri la Alphonse Lusako dhidi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu (CAG) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

b. Shauri la Skymax Elevators Limited dhidi ya Mwanasheria Mkuu na Wenzake; na

c. Shauri la Jeremiah Mtobesya na mwenzake dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu kifungu Na. 148 (5) cha Kanuni ya Adhabu (Penal Code).

**Ndugu wajumbe wa Baraza;**

Katika mwaka wa fedha 2023/24, Ofisi imesajili na kuendesha jumla ya Mashauri ya madai takribani **9,650** kati ya Mashauri hayo, Mashauri **9,519** ni ya kitaifa (zaidi ya asilimia 60 ni mshauri ikiwa ni migogoro ya ardhi) na Mashauri **131** ni ya kimataifa. Katika kuendesha Mashauri hayo, Mashauri **1,412** yalimalizika. Ambapo kwa kumalizika kwa Mashauri hayo, Ofisi imeokoa jumla ya shilingi za kitanzania **Bilioni Mia Tano Thelathini na Sita na Nukta Tano (536,515,717,327)**.

**Ndugu wajumbe wa Baraza;**

Katika kipindi hicho hicho, cha Mwaka wa fedha 2023/24, Ofisi imeshughulikia jumla ya Mashauri ya usuluhishi **201** ambapo, kati ya Mashauri hayo, Mashauri **170** ni ya usuluhishi wa ndani na Mashauri

**31** ni ya usuluhishi wa kimataifa. Kati ya Mashauri **201** yaliyoshughulikiwa, Mashauri **43** yamemalizika kwa njia ya majadiliano, mahakamani na kwenye Mabaraza ya Usuluhishi.

Kumalizika kwa mashauri haya, Ofisi imeokoa jumla ya ***shilingi Bilioni Sitini na Sita nukta Sifuri Mbili*** (**66,020,015,593.38),** Dola za Marekani ***Milioni Mia Nane Nukta Mbili*** (**817,643,693.12)** na **EURO *Milioni Mbili* (2,000,000)**.

## Ndugu Wajumbe wa Baraza;

Kwa upande wa wafanyakazi, kumekuwa na maboresho katika mazingira ya kazi, hususan katika kuongeza rasilimali watu na vifaa vya kufanyia kazi kama alivyotoka kuelezea Makamu Mwenyekiti kwenye Hotuba yake. Hata hivyo, changamoto bado zipo, kama vile ukosefu wa rasilimali katika baadhi ya idara na uhitaji wa kuongeza ujuzi kwa wafanyakazi. Tunazifanyia kazi na tutaziboresha.

## Ndugu Wajumbe wa Baraza;

Naomba niwashukuru sana kwa kazi nzuri mnazofanya ili kuhakikisha kuwa Ofisi hii inatekeleza majukumu yake ipasavyo, mafanikio tunayoyapata kwenye kila hatua ni yetu sote. Hivyo ni rai yangu kuwa mtaendelea na hari hiyo hiyo na kufanya kazi kwa bidii, weledi na kwa kuzingatia misingi ya utumishi wa Umma.

Katika Mwaka wa Fedha 2024/ 25 Ofisi yetu inaendelea na mikakati mbalimbali ya kutatua changamoto zilizobainishwa ili kuboresha utendaji kazi wetu. Sisi wote ni mashahidi kuwa kwa kipindi hiki kidogo cha mwaka huu wa fedha tumechukua hatua mbalimbali za kuboresha maslahi ya watumishi na utendaji kazi wetu kwa ujumla. Hatua hizo zinajumlisha masuala yafuatayo;-

a) Kuweka mipango mikakati kwa ajili ya utoaji wa mafunzo ya ubobezi kwa mawakili kwenye masuala mbalimbali ikiwemo masuala ya gesi na madini, masuala ya mikataba ya ujenzi na masuala ya Usuluhishi wa kimataifa. Tunatarajia kuanza mafunzo hayo mapema mwezi Novemba, 2024 na mafunzo hayo yatakuwa ni endelevu;

b) Kama tutakavyojadili leo hii, Ofisi inaendelea kuboresha maslahi ya watumishi kupitia maboresho ya miundo pamoja na mikakati mbalimbali inayoendelewa kuwekwa na Ofisi;

c) Vilevile, Ofisi inaendelea kuboresha na kuweka mifumo rafiki ya usimamizi wa Mashauri ili kurahisha utoaji wa Taarifa za Ofisi na kuboresha utendaji kazi wetu.

Hayo ni mafanikio machache tu tuliyopata kwenye kipindi kifupi cha mwaka huu wa fedha. Tunatarajia kufanya mengi zaidi na kwenye Baraza lijalo tutatoa taarifa kamilifu ya mafanikio tuliyopata kwenye mwaka huu wa fedha.

## Ndugu Wajumbe wa Baraza;

Sanjali na hayo, nimeelezwa pia kuwa hapo kesho mtapata wasaa wa kupata mafunzo katika masuala mbalimbali ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yenu ya kila siku kwa weledi mkubwa zaidi.

Aidha, mafunzo hayo yatahusisha ;-

i. Masuala ya Udhibiti wa Msongo wa Mawazo ***(Stress Management)***;

ii. Maandalizi ya Kustaafu katika Utumishi na Uongozi ***(Retirement Plan)*** ; na

iii. Dhana ya Ujumuishi wa Anuai za Kijamii ***(Workforce Diversity and Inclusion)*** sehemu za kazi.

Maada hizi ni muhimu sana katika utendaji kazi wetu. Hivyo, nawasihi mtumie muda huu vizuri, msikilize kwa umakini, na kuhakikisha kuwa mnajifunza kwa kina ili kufikia manufaa yatakayowasaidia sasa na baadae.

## Ndugu Wajumbe wa Baraza;

Kama mnavyokumbuka kuwa mwezi Novemba mwaka huu nchi yetu inatarajia kushiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Mtakubaliana nami kuwa Uchaguzi wa Serikali za mitaa ni muhimu katika jamii na

utawala kwa kuwa uchaguzi huu ndio kiungo muhimu katika kuhakikisha Serikali inaweka miundombinu chanya ya huduma za kijamii kwa kuzingatia uwiano sawa na wananchi waliopo katika eneo husika.

Ofisi itakuwa na jukumu la kusimamia kesi zitakazotokana na uchaguzi. Hivyo, tunajukumu la kufanya kazi hiyo kwa weledi.

Hivyo, naomba hadhira hii kujiandikisha na kutumia nafasi na fursa hii ya kikatiba kuweza kuchagua viongozi sahihi kwenye mitaa yetu watakaosaidia kutuletea maendeleo kwa wakati.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, nipende kushukuru na kuipongeza Kamati ya Maandalizi chini ya Usimamizi madhubuti wa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuratibu kikao hiki cha Baraza la Wafanyakazi. Vilevile niwashukuru wajumbe kutoka TUGHE Mkoa wa Dar es Salaam, kwa kufanya kazi kwa karibu na Tawi la TUGHE la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha Baraza hili la Wafanyakazi linafanya kazi kama inavyotakiwa.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Naomba nimalizie kwa kuzungumzia masuala yafuatao;-

i. Naahidi kufanya kazi kwa bidii kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zinaongoza Ofisi hii;

ii. Kufanya kazi kwa umoja, mshikamano na upendo wa hali ya juu;

iii. Wote tuhakikishe kuwa tunalinda maslahi mapana ya nchi yetu;

iv. Maslahi ya Watumishi wa Ofisi. Viongozi tusiwakandamize watumishi wetu;

v. Tujali kada zote za watumishi;

vi. Umuhimu wa Kada zote;

vii. Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo wafanye kazi kwa umahiri Zaidi;

viii. Kudumisha ushirikiano na umoja katika kutekeleza majukumu kwa mashirikiliano na taasisi nyingine;

ix. Uharaka wa kufanya na kutatua changamoto za watumishi;

x. Open door policy- kuwa tayari kusikiliza changamoto za watumishi na kutafuta utatuzi;

xi. Kuinuana – kusogezana usimbanie mtu mwenye kipaji au talent;

xii. Maboresho ya Muundo na maslahi ya watumishi;

xiii. Ofisi kutafuta viwanja kwenye ofisi za kanda kama Mbeya, Arusha na Mwanza;

xiv. Tujifunze kwenye mifumo na Teknolojia—Tuko kwenye michakato ya kuboresha mifumo wa CIMS;

xv. Career growth- ni vyema kuwa mbobezi kwenye eneo Fulani, kuelekeza wasome;

Ninapohitimisha hotuba hii, naomba kuwasihi sote tuendelee kushirikiana na kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili kuhakikisha tunafikia malengo yetu. Mafanikio ya ofisi yetu yanategemea sana bidii na uadilifu wa kila mmoja wetu. Tutambue kuwa mafanikio ya leo ni matokeo ya juhudi za pamoja na changamoto tulizozikabili.

Baada ya kusema haya, sasa natamka rasmi kuwa Mkutano wa Kwanza wa Baraza la Pili la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 umefunguliwa rasmi.

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA.**

**MUNGU IBARIKI OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI!**

**MUNGU IBARIKI TANZANIA!**